

## SERIKALI KUTOA KOMPYUTA NA PRINTA KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZILIZO NDANI YA MKOA WA KAGERA

Naibu Waziri wa Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari **MHESHIMIWA KUNDO ANDREA MATHEW** amesema Serikali ya Jamhuri ya Tanzania inatazamia kutoa jumla ya kopyuta arobaini na tano (45) na printa tisa (9) katika shule tisa za Sekondari zilizo ndani ya Mkoa wa Kagera zikiwemo shule tatu kutoka Halmashauri ya Wilaya Bukoba ambazo ni Shule ya Sekondari Kashanje, Kabale na Buzi. Komyputa hizi zinatazamiwa kuzifikia shule hizo ndani ya miezi miwili toka tarehe 30.7.2021.

Mheshimiwa Naibu Waziri ameyasema hayo wakati alipokuwa akizungumza na maafisa TEHAMA wa Halmashauri ya Wilaya Bukoba na Manispaa ya Bukoba, Mkuu wa Wilaya Bukoba, Katibu Tawala Mkoa Kagera, Mkuu wa Mkoa Kagera na wadau wa mawasiliano katika ukumbi wa mkutano wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Kagera ambapo pia alieleza kwamba lengo la utoaji wa kompyuta hizo ni kusukuma mbele gurudumu la TEHAMA nchini na kuwapa uzoefu vijana wanaotoka katika familia za kawaida ili wanapofika vyuo vikuu wasiwe wageni wa kutumia kompyuta katika shughuli zao za kimasomo.



Aidha Mheshimiwa Naibu Waziri ameagiza maafisa TEHAMA wote waliomo katika Ofisi za taasisi za Serikali wahakikishe wamesajiliwa na Tume ya Usajili ya TEHAMA ili waweze kuwa na sifa ya kuendelea kufanya kazi za TEHAMA katika taasisi zao kwa kuwa itafika wakati ambapo Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari haitawaruhusu maafisa TEHAMA ambao hawajasaliwa na tume hiyo kufanya kazi yote inayohusiana na TEHAMA katika Halmashauri na taasisi za Serikali na amesema kwamba usajili huo utatanguliwa na mtihani kwa wanaoomba kusajiliwa na kufaulu kwao mtihani huo ndio kutawafanya wapate usajili.

Kwa upande mwingine mheshimiwa Naibu Waziri alizungumzia kuhusu suala la mfumo wa anuani za makazi ambapo aliipongeza Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba kwa kujitahidi kutengeneza mfumo huo ndani ya eneo lake kwa kutumia mapato yake ya ndani jambo ambalo limeifurahisha Serikali na kuamua kuiunga mkono Manispaa hiyo kwa kuitengea milioni mia tisa(900,000,000/=) ili

kuiongezea nguvu katika uendelezaji wa zoezi hilo na akazitaka Halmashauri zingine za mkoa wa Kagera kuongeza bidii pia katika ufanikishaji wa zoezi hilo la uwekaji wa mfumo wa anuani za makazi katika maeneo yao kwani ukamilishaji wa zoezi hilo utazisaidia Halmashauri kukusanya kwa urahisi mapato kwa kuwa anuani hizo zitakuwa zinaonesha jina la mtu na eneo analopatikana lakini pia zitarahisha mawasiliano na kupunguza adha ya wageni kupotea pindi wanapotaka kwenda eneo moja hadi lingine.

Mwisho Mheshimiwa Naibu Waziri alisema Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika mwaka huu wa fedha 2021/2022 imetenga zaidi ya shilingi bilioni moja kupitia mfuko wa Mawasiliano kwa umma kwa ajili ya kutekeleza miradi ya mawasiliano katika vijiji sitini na tano (65) vilivyomo ndani ya Mkoa wa Kagera katika Wilaya za Misenyi, Kyerwa, Ngara na Karagwe na zaidi ya shilingi bilioni mia mbili zimetengwa kwa ajili ya kuboresha zaidi ujenzi wa mkongo wa taifa na kwamba Wizara ya Mawasiliano imeazimu kwamba itatumia wakandarasi wa ndani ya nchi katika kutekeleza miradi yake yote ili kusaidia kukuza uchumi wa wananchi na taifa kwa ujumla.

Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ni Wizara iliyoungwa mnamo Desemba 5 mwaka 2020 ikimeguliwa toka katika Wizara ya Ujenzi Uchukuzi na Mawasiliano na inahudumia taasisi sita ambazo miongoni mwake ni Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Shirika la Mwasiliano Tanzania (TTCL), Shirika la Posta na Kitengo cha TEHAMA.

*Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya Bukoba ndugu Solomon Kimilike akifuatilia kwa ukariu hotuba ya Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.*

